



## BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

### ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

#### BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

#### MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Tatu – Tarehe 09 Mei, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.

#### I. TAARIFA YA SPIKA:

#### II. MASWALI:

#### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

208. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba,  
Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Sheria inazungumzia vipi juu ya watoto wanaotenda makosa  
makubwa wakiwa chini ya umri wa miaka 18.

#### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

90. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na  
Mipango:

Kwa kiasi gani wastaafu wanawezeshwa kuwekeza kwenye taasisi  
za kifedha.

### **Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

88. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni lini Wizara yako italitatu tatizo la upatikanaji na usogezaji wa maduka ya pembejeo karibu na maeneo ya shughuli za kilimo za wananchi.

### **Wizara ya Afya:**

24. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ongezeko la maduka ya dawa limerahisisha kupatikana dawa za binadamu, lakini pia limeongeza hatari ya madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi hayo. Hali hii imapelekeea tatizo kubwa la utumiaji wa dawa kiholela.

- (a) Kwa tathimini ya Serikali, hali ya kutumia dawa kiholela iko vipi nchini mwetu.
- (b) Ni miongozo gani ya kitaalamu ambayo Serikali imetoa kwa maduka ya dawa ili kupunguza athari za kutumia dawa kiholela.
- (c) Ni athari zippi zinazoweza kutokea kutokana na kutumia dawa hizi za binadamu kiholela.

### **Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

106. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

- (a) Kuna kauli mbiu ngapi zimeweza kutumika katika kuiendeleza na kuzidi kuiimarisha lugha adhimu ya Kiswahili.
- (b) Je, kwa kiasi gani kauli mbiu hizo zimekuwa na tija na mafanikio.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

248. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Miongoni mwa juhudii kubwa zilizofanywa na Serikali yetu, ni pamoja na kuimarisha suala la uvuvi, ikiwa ni pamoja na uzalishaji na uvunaji wa samaki.

- (a) Je, ni kwa kiasi gani mahitaji ya samaki kwa mwaka yanaendana na uwezo wa uzalishaji na uvunaji wa samaki nchini.
- (b) Je, muwamko wa wananchi uko vipi juu ya uzalishaji na uvunaji wa samaki nchini.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2025/2026.

Zanzibar,  
09 Mei, 2025.

  
(Raya Issa Msellellem)  
**KATIBU WA BARAZA**